

HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Singida:

Simu : 0262 – 964037/6

Baruapepe: ded.ikungidc@singida.go.tz

Tovuti: www.ikungidc.go.tz



S.L.P. 42,

SINGIDA.

Kumb. Na. IDC/B.1/8/A/30

Tarehe: 26 Oktoba, 2020

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi anapenda kuwatangazia waombaji wenye sifa kujaza nafasi ya kazi ya **Katibu Mahsusi Daraja la III**.

1 KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III - NAFASI MOJA (1).

a) Sifa za kuingilia moja kwa moja:-

- i. Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha Nne (Form IV) waliohudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft office, Internet, E-mail na Publisher.
- ii. **Umri 18- 45**

b) Kazi/Majukumu ya kufanya:

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/ kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

MSHAHARA:

Ngazi ya Mshahara wa Serikali TGS. B

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI:-

- i. Waombaji kazi wote waombe kwa kufuata masharti ya **TANGAZO LA KAZI**,
- ii. Waombaji kazi wote wawe raia wa Tanzania .
- iii. Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) zenye mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu,
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo
 - a) Cheti cha Mafunzo ya Uhazili
 - b) Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita,
 - c) Cheti cha kuzaliwa.
- v. Hati ya matokeo ya kidato cha nne au sita (Result slip) haitafanyiwa kazi,
- vi. Kuwasilisha vyeti vya kughushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za Kisheria.
- vii. Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- viii. Waombaji waonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao, anuani na namba za simu.
- ix. Waombaji kazi wenye vyeti vya kidao cha nne na cheti cha Taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (**NECTA**) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (**NACTE**).
- x. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
- xi. Watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.
- xii. Waombaji kazi ambao maombi yao hayakukidhi vigezo vya tangazo hayatafanyiwa kazi.

Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni **tarehe 13 Novemba, 2020 saa tisa na nusu (9:30) Alasiri.**

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi,

S.L.P. 42,

SINGIDA.

Justice L. Kijazi
MKURUGENZI MTENDAJI